*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 80-97*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.5

# Athari za Mabadiliko ya Maana katika Lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka Matini za Kidini

*Lydiah S. Mwenje*[1] na *Stanley A. Kevogo*[2]

## Ikisiri

Makala hii inachanganua matumizi ya lugha katika mahubiri ya kidini. Azma kuu ni kuchunguza jinsi maana za maneno zinavyobadilika kiisimu zinapotumiwa kwenye miktadha ya mahubiri ya Kikristo. Data ya utafiti imetokana na unukuzi kimaandishi wa vipindi 5 vya mahubiri ya Kikristo yaliyorekodiwa kati ya Mei na Agosti, 2020 kutoka idhaa tatu za runinga nchini Kenya, yaani KBC, SAYARE na MBCI. Wahubiri 5 waliotumia Kiswahili tu kwenye vipindi vya idhaa hizi ndio walioteuliwa kwa usampulishaji kusudio. Data ya semi 64 zilizoteuliwa kwa usampulishaji huo zilichanganuliwa kwa mwongozo wa madhumuni ya utafiti pamoja na mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Matokeo yanaonesha kwamba baadhi ya maneno yaliyotumiwa na wahubiri wa dini za Kikristo huwasilisha maana kipragmatiki. Maana za maneno hayo kimatumizi ni tofauti na maana msingi. Aidha, uchunguzi huu unaazimia kuendeleza mtazamo wa isimu kuhusu jinsi matumizi ya lugha katika muktadha wa sajili hii maalumu unavyoathiri mawasiliano.

## 1.0 Utangulizi

Lugha ni nyenzo muhimu ya mawasiliano miongoni mwa jamii za wanadamu. Hufanikisha shughuli nyingi za kila siku zikiwamo elimu, biashara, siasa na dini. Pamoja na lugha kuwa kiungo muhimu kwa binadamu duniani, dini pia ina dhima muhimu katika jamii (Malugu, 2016). Wanadamu huitumia lugha kufanikisha shughuli za kidini ikiwamo kusali, kuimba na kuwasilisha mahubiri. Upekee wa matumizi ya lugha ibadani na kwenye miktadha ya kidini kwa ujumla, unalifanya kuwa suala muhimu kuchunguzwa na wanaisimu.

[1] Mzamivu, Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya. Baruapepe: lydia.mwenje@gmail.com

[2] Mhadhiri, Idara ya Lugha, Taaluma za Fasihi na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia, Kenya. Baruapepe: sadika@jooust.ac.ke

Uhusiano wa lugha na dini hujitokeza wazi kiisimu ikizingatiwa kwamba lugha ni nyenzo ya kueneza dini (Kevogo, 2020). King'ei (2010) anafafanua kwamba lugha ya kidini huathiriwa sana na utamaduni ulioiasisi dini husika. Kila dini aghalabu huwa na imani na utamaduni unaoipambanua katika uendelezaji wa shughuli zake ambazo nazo huathiri matumizi ya lugha. Matumizi ya lugha hutegemea muktadha ambao huathiri maana katika mawasiliano yanayohusika. Ufanisi wa mawasiliano katika matumizi ya lugha yoyote ile hutegemea jamiilugha inayohusika. Mawasiliano halisi hutokea tu pale ujumbe unapofasirika kwa usahihi na kwa maana iliyokusudiwa na mtungaji (King'ei, 2010; Holmes na Wilson, 2022).

Suala la dini husawiriwa kwa njia tofautitofauti ambazo ni chanya na hasi. Tafiti za awali zimeangazia matumizi ya lugha na dini katika mitazamo tofauti. Nyingi katika tafiti hizo zimechunguza matumizi ya lugha katika dini za Kiislamu na Kikristo ilhali nyingine zimeangazia uhusiano wa dini na fasihi. Mathalani, Beja na Mwinyifaki (2013) wamechunguza dini ya Kiislamu naye Chembea (2020) ameonesha uhalisia ajabu unavyodhihirika katika ushairi wa Kiswahili na namna uanavyoendeleza maudhui ya dini ya Kiislamu. Mpalanzi (2019) ameshughulikia makutano kati ya dini za jadi na dini za kigeni akirejelea riwaya teule za Kiswahili. Nao Osore (2015) na Malugu (2016) wakiangazia dini ya Kikristo, wameonesha uhusiano wa fasihi na dini ambapo Osore (2015) amechunguza fasihi andishi ya Kiswahili na dini na Malugu (2016) ameshughulikia nafasi ya fasihi katika kusawiri suala la dini. Akitofautiana nao kinadharia, Marisya (2017) kwa mtazamo wa Pragmatiki Leksika, amechunguza uhusiano kati ya fasihi andishi na dini kwa kurejelea riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea* na *Ndoto ya Almasi*. Utafiti huu unatofautiana na tafiti hizi kwa sababu unaangazia mahubiri ya dini ya Kikristo kwa mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Kwa hivyo, makala hii inachanganua kipragmatiki, jinsi maana za maneno zinavyorekebishwa kimatumizi kwenye miktadha ya mahubiri ya Kikristo.

## 2.0 Uhakiki wa Maandishi

Tafiti mbalimbali zimeshughulikia suala la lugha na dini kwa mitazamo tofautitofauti. Indende (2007) akiongozwa na Nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975), ametathmini lugha ya kitamathali katika mahubiri ya dini ya Kikristo. Kwa kuangazia tamathali za usemi, utafiti wake unaonesha baadhi ya tashbiha na sitiari zinazotumiwa katika dini ya Kikristo kwa ujumla. Ingawa utafiti wa Indede (2007) unahusu mahubiri ya Kikristo, umejikita pia kwenye mtindo wa matumizi ya lugha ilhali utafiti huu wa sasa unachanganua kipragmatiki baadhi ya maneno katika matini ya kidini kwenye idhaa za runinga teule.

Ogutu (2013) amechunguza athari zinazosababishwa na matumizi ya *Sheng* katika dini ya Kikristo katika Mtaa wa Umoja, Jijini Nairobi. Imebainika kwamba Sheng imesababisha mgogoro unaoendelea kati ya wanajamiilugha wa *Sheng* na

wanajamiilugha wengine ambao pia ni waumini wa dini ya Kikristo. Matumizi ya *Sheng* kanisani yanahusishwa na athari hasi na chanya. Kwa mfano, makanisa yanayotumia lugha ya *Sheng* katika ibada zao yameishia kuhudhuriwa na waumini wengi ambao ni vijana. Utafiti wa Ogutu ulijibana kwenye athari za lugha ya *Sheng* katika dini ya Kikristo. Hata hivyo, makala hii inaangazia jinsi muktadha wa Kikristo unavyoathiri maana ya baadhi ya maneno ya Kiswahili katika mahubiri ya Kikristo.

Matatizo ya kiisimu yanayojitokeza katika ukalimani wa mahubiri ya kidini yameshughulikiwa na Ogonda (1998). Matatizo yaliyodhihirishwa ni ya kifonolojia, kifonetiki, kileksika na ya kisintakisia. Pamoja na hayo, matatizo yasiyo ya kiisimu, kama vile matumizi ya ujumbe mrefu, mwendo wa kasi na hisia za mkalimani yameonesha kuathiri ujumbe unaowasilishwa kwenye mahubiri. Kwa upande mwingine, Nthenya (2012) pamoja na Odhiambo na wenzake (2013) wamechunguza athari na mikakati ya mawasiliano inayotumiwa na wakalimani katika makanisa teule ya Kipentekoste Mjini Machakos. Wameonesha jinsi ukalimani kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kikamba unavyoweza ama kufanikisha au kutatiza mawasiliano. Ingawa tafiti hizi tatu zinahusu uhawilishaji wa maana na ujumbe kwa njia ya ukalimani kwenye miktadha ya dini ya Kikristo, zinatofautiana na utafiti huu wa sasa unaochunguza dhima ya muktadha wa mawasiliano kama mojawapo ya vipengele vinavyoathiri maana inayowasilishwa na maneno yatumikayo kwenye mahubiri ya Kikristo.

Mutiso (1996; 2005) na Okombo (2011) wameshughulikia mtindo katika matini za ushairi wa kale unaosawiri dhamira za dini ya Kiislamu. Katika uchunguzi wake, Okombo (2011) ameachunguza matumizi ya sitiari, taashira na tashbiha katika *Utenzi wa Tambuka* kuwasilisha ujumbe unaohusu dini ya Kiislamu. Akilenga ishara na uashiriaji anuwai unaopatikana katika shairi la *Kaswida ya Burudai,* Mutiso (1996) amejishughulisha na umboasili la motifu katika ushairi wa Kiislamu. Ijapokuwa tafiti hizi zimekitwa kwenye mtindo wa lugha katika matini zinazowasilisha dhamira za dini ya Kiislamu, zimeinufaisha makala hii kwa sababu maana inayowasilishwa na baadhi ya maneno hueleweka kimuktadha kutokana na vipashio vya kiisimu vinavyotumiwa kuwasilisha mahubiri ya kidini kwa ujumla.

Marisya (2017) akiongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika, amefafanua uhusiano uliopo baina ya matini za kifasihi andishi na dini ya Kikristo. Pamoja na mambo mengine, amedhihirisha uwezo wa sajili ya dini ya Kikristo kuwasilisha maudhui, dhamira pamoja na kujenga wahusika kwa ufanisi kwenye matini za riwaya zinazoshughulikiwa. Kinadharia, utafiti wa Marisya unahusiana na huu. Hata hivyo, tofauti ipo katika aina za matini zilizochanganuliwa, yaani riwaya teule za Ken Walibora na mahubiri ya Kikristo yalirekodiwa kwenye idhaa teule za runinga.

Kevogo na Kevogo (2018) wamechunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufanikisha mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii kwa kuzingatia blogu za Kikristo. Wakiongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (Fairclough na Wodak, 1997; Fairclough, 2003), wanadadavua mchango wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye blogu za Kikristo katika kuenea kwa lugha ya Kiswahili duniani. Imethibitika kwamba watumiaji wa blogu za Kikristo wanaowasiliana kwa Kiswahili hutumia misimu na misemo, huchanganya na kubadili msimbo na kutumia vifupisho visivyo sanifu. Fauka ya haya, wanahitimisha kwamba matumizi ya Kiswahili kwenye blogu za Kikristo yanachangia kueneza Kiswahili duniani kwa kutoa fursa kwa watumiaji wa blogu walio nje na ndani ya Afrika Mashariki kujifunza na kuimarisha matumizi yao ya lugha. Ingawa utafiti huu pia unachanganua matini za Kiswahili kwenye miktadha ya vyombo vya habari vya kielekroniki, tofauti ipo katika misingi ya kinadharia na madhumuni ya utafiti. Aidha, utafiti wao haujihusishi moja kwa moja na kipengele cha maana inayowasilishwa na vipashio vya kiisimu vilivyochunguzwa.

Kwa kutumia mkabala mseto wa Nadharia ya Ushikamani (Halliday na Hasan, 1976), Nadharia ya Tendo Uneni (Austin, 1962; Searle, 1969) na Nadharia ya Umaanisho (Grice, 1975), Kingati (2002) ameshughulikia lugha inayotumika katika mahubiri ya Kanisa Katoliki jijini Nairobi. Amechunguza muwala, ushikamani, ubora wa utendaji na maana ya kipragmatiki katika matini teule za mahubiri ya Kiswahili. Ingawa misingi ya kinadharia, malengo na miktadha ya uchunguzi ni tofauti, utafiti huu una tija kwa makala hii kwa sababu unashughulikia mahubiri kwa mtazamo wa kiisimu. Aidha, maana ya kipragmatiki katika mahubiri ya Kikristo ya Kiswahili imeshughulikiwa kwa ujumla bila kuhusisha uchanganuzi wa vipashio mahususi vya kileksika.

Waweru (2014) amechanganua ubadilishaji msimbo katika mahubiri ya Kanisa Katoliki. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Umaanisho (Grice, 1975), amechambua data ya matini iliyorekodiwa kwenye ibada za makanisa teule matatu. Imethibitika kwamba katika mahubiri yao, wahubiri katika ibada za Kanisa Katoliki hubadilisha msimbo kwa wingi. Ubadilishaji msimbo katika mahubiri ya Kikristo, aghalabu, huathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu. Pamoja na ubadilishaji msimbo kusababisha ukosefu wa urasmi, elimu, tabaka, tajriba, cheo na umri pia husababisha mabadiliko katika matumizi ya lugha. Ijapokuwa Waweru anachanganua data iliyotokana na matini ya mahubiri ya Kikristo, miktadha ya mawasiliano, misingi ya kinadharia, azma na madhumini mahsusi ni tofauti na ya utafiti huu. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika, tunachanganua jinsi muktadha wa dini ya Kikristo unavyoathiri maana katika baadhi ya maneno katika mahubiri.

## 3.0 Nadharia ya Pragmatiki Leksika

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika iliyoasisiwa na Blutner katika miaka ya 1990. Nadharia hii huchunguza jinsi maana ya neno inavyobadilishwa katika matumizi. Katika nadharia hii, maneno yanahakikiwa katika utaratibu fulani na kufasiriwa kulingana na muktadha fulani maalumu. Chimbuko la Nadharia ya Pragmatiki Leksika ni Semantiki Leksika na Pragmatiki Leksika. Semantiki Leksika huchunguza uhusiano kati ya neno na dhana inayosimbwa ilhali Pragmatiki Leksika inaeleza kwa nini wazo limewasilishwa kwa kutumia neno linalotofautiana na dhana iliyosimbwa.

Blutner (2011) anadai kuwa wazo la kimsingi kuhusu Pragmatiki Leksika liliasisiwa na McCawley (1978). McCawley akigusia kanuni za mazungumzo za Grice (1967) katika Cole na Morgan (1975), anaonesha kwamba tofauti kati ya muundo wa isimu wa maana iliyosimbwa na fasili iliyopendekezwa ni matokeo ya kanuni za jumla za tabia za ushirikiano na huenda kwa hatua zinazotabirika. Akiwarejelea Katz na Fodor (1963), Blutner (2004) anahoji kwamba maana ya neno aghalabu hutegemea muktadha wa sentensi linamotumika. Nao Katz na Fodor (1963) wanaeleza kuwa muktadha unahusu habari za awali, mambo ya kijamii na maarifa ya kiisimu. Wanasisitiza zaidi kuwa, maana kamilifu ya neno inapaswa kuhusisha habari zaidi inayomwezesha mtu kupambanua maana za maneno anuwai.

Blutner (2004) aneleza vipengele mbalimbali vinavyoshughulikiwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Vipengele vyenyewe ni pamoja na pragmatiki ya vivumishi, athari za uimarishaji hasi, utaratibu wa polisemia na matukio mengi yanayojadiliwa ndani ya mfumo wa semantiki tambuzi. Pragmatiki Leksika huchunguza taratibu ambazo kwazo maana za maneno zilizobainishwa kiisimu hurekebishwa katika matumizi. Akiwarejelea Wilson (2003) na Carston (2002), Blutner (2011) anabainisha michakato mitatu ya kisemantiki inayohusiana na utafiti huu. Michakato yenyewe ndiyo mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Mchakato wa kwanza ni ufinyazi wa maana ya neno linalohusika. Hii ni hali ambayo neno linatumika kueleza maana finyu kuliko maana iliyosimbwa. Hivyo, maana finyu ni sharti iwe inahusiana na muktadha wa matumizi ya neno hilo. Mchakato wa pili ni upanuzi wa maana ya neno. Hali ambayo neno lenye maana finyu linatumika kuwasilisha maana ya jumla. Mchakato wa mwisho ni ukisiaji wa maana ya neno. Hali ya ufasiri ambapo neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu kinachohusiana nacho na ambacho kina maana tofauti na maana msingi ya neno hilo.

Mihimili hii mitatu ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika inatuongoza katika uchambuzi wa data zinazohusisha baadhi ya maneno katika mahubiri yaliyorekodiwa. Maneno yenyewe yamechambuliwa kwa misingi ya michakato ya

maana ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika ambayo ni ufinyazi wa maana, upanuzi wa maana na ukisiaji wa maana.

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu wenye muundo wa kiuchanganuzi umewasilishwa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo huhusisha ukusanyaji wa data na kuzichambua kwa njia ya ufafanuzi (Nassaji, 2015). Data zimekusanywa kati ya Mei na Agosti, 2020 kwa njia ya kurekodi mahubiri katika lugha ya Kiswahili. Vipindi vitano vya idhaa tatu za runinga, yaani KBC, MBCI na SAYARE viliteuliwa. Vipindi hivyo ni sampuli wakilishi ya mahubiri yanayotazamwa kwenye idhaa hizo tatu za runinga. Idhaa hizi 3 ziliteuliwa kwa usampulishaji kusudio kwa sababu hurusha vipindi vya mahubiri yawasilishwayo kwa lugha ya Kiswahili. Wahubiri 5 waliohubiri kwa Kiswahili katika vipindi vya idhaa hizi tatu ndio walioteuliwa kwa usampulishaji kusudio pia.

Kurekodi data za mahubiri kutoka kwenye vituo vya runinga kulitufaa kwa sababu mahubiri yaliwasilishwa kwenye mazingira, miktadha na hali halisi pasipo kufanyiwa ukarabati wowote. Matini za mahubiri zimerekodiwa kwa kutumia kinasa sauti na kunukuliwa baadaye kimaandishi. Data zilizonukuliwa kimaandishi zimechanganuliwa kwa umakini, kisha uteuzi wa sampuli kusudio ya maneno 64 yaliyotumika umefanywa kwa mwongozo wa madhumuni ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data umetekelezwa kimaelezo.

## 5.0 Uchanganuzi wa Maneno ya Kidini Kipragmatiki

Uchanganuzi wa data umeongozwa na madhumuni ya utafiti pamoja na mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Kwa mujibu wa Blutner (2011), akiwarejelea Wilson (2003) na Carston (2002), mambo ya msingi yanayoshughulikiwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika huainishwa katika kumbo tatu. Mambo haya ndiyo yaliyoongoza uchanganuzi wa maneno katika mahubiri ya Kikristo, yaani, ufinyazi wa maana, upanuzi wa maana na ukisiaji wa maana.

Uchanganuzi wa mambo haya matatu umebainisha kuwa upanuzi wa maana ndio uliojitokeza kwa wingi. Ufinyazi wa maana pia ulijitokeza kisha ukisiaji wa maana ukajitokeza kwa uchache zaidi, kama inavyowasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mdafao wa Kumbo la Semi katika Mahubiri**

| Mhusika | Maana ya Neno | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | Kupanuka | Kufinywa | Kukisiwa | |
| Mhubiri wa 1 | 11 | 01 | 00 | 12 |

| **Mhusika** | **Maana ya Neno** | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | **Kupanuka** | **Kufinywa** | **Kukisiwa** | |
| Mhubiri wa 2 | 15 | 01 | 03 | 19 |
| Mhubiri wa 3 | 09 | 02 | 02 | 13 |
| Mhubiri wa 4 | 04 | 02 | 00 | 06 |
| Mhubiri wa 5 | 12 | 02 | 00 | 14 |
| **Jumla** | **51** | **08** | **05** | 64 |

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Jedwali Na. 1 linaonesha idadi ya wahubiri waliorekodiwa na jumla ya idadi ya maneno yaliyotumika na kuonesha kupanuka, kufinywa na kukisiwa kwa maana. Imebainika kuwa maneno mengi yameonesha kupanuka kwa maana, yaani maneno 51; kufinywa kwa maana maneno 8, kisha kukisiwa kwa maana maneno 5. Kwa ujumla, maneno yote yalikuwa 64.

### 5.1 Kupanuka kwa Maana

Upanuzi wa maana ni kitendo cha kulipa neno au maneno maana ya ziada (Jilala, 2017). Hii ni hali ambayo neno linalorejelea kitu kimoja katika hali ya kawaida linatumika kurejelea maana pana zaidi ya maana iliyosimbwa kisemantiki katika neno hilo. Kutokana na uchanganuzi wa mahubiri yaliyonukuliwa kimaandishi, maneno 51 kati ya 64 yameonesha kupanuka kimaana. Mifano 5 ya maneno yaliyoonesha kupanuka kwa maana yamewasilishwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Kupanuka kwa Maana**

| **Msamiati au Neno** | **Maana ya Kiisimu** | **Maana ya Kimuktadha** |
|---|---|---|
| **Upanga** | Chuma kirefu chenye ncha na makali pande zote mbili kinachotumiwa kuwa ni silaha. | Neno la Mungu |
| **Inua** | Kuleta juu kitu kilicho mahali palipo chini | Kubadilika kutoka katika hali duni na kuwa katika hali bora |
| **Njia** | Barabara au kichochoro inayotumiwa ili kupitia | Yesu Kristo kama njia ya kwenda mbinguni |
| **Utu wa kale** | Utu ni hali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya mtu ilhali kale ni zama zilizopita, zamani au dahari. Kwa hivyo, utu wa kale ni ubinadamu wa zamani. | Hali ya uovu |

| Msamiati au Neno | Maana ya Kiisimu | Maana ya Kimuktadha |
|---|---|---|
| **Urembo** | Ni uzuri, umaridadi | Kubadilika kutoka katika hali duni na kuwa bora |
| **Vita** | Mapigano baina ya watu, wanyama au mataifa | Hali ya kuzuia kutendeka kwa jambo kwa vitendo au maneno. |

**Chanzo:** TUKI (2019) na Uwandani (2020)

Neno ‘upanga’ lilitumiwa na mhubiri kwa namna mbili zilizosawiri upanuzi wa maana. Upanga ni ‘chuma kirefu chenye ncha na makali aghalabu pande zote mbili kinachotumiwa kuwa ni silaha’ (TUKI, 2019: 691). Maelezo haya yana maana kuwa ‘upanga ni silaha au kifaa’. Hata hivyo, katika muktadha wa mahubiri haya, upanga umehusishwa na maovu ambayo mtu anaweza kumtendea mtu mwingine ambaye ni adui yake. Baadaye, maovu hayo humgeukia na kumdhuru mwenyewe. Jinsi upanga unavyotumika kama kifaa cha kukata kwa pande zote, unalinganishwa na maovu ya binadamu yanayomdhuru mwenyewe baadaye. Maana ya upanga, kama kifaa cha kukata, imepanuka na kutumika kuonesha maovu.

Neno ‘upanga’ lilitumiwa tena kwa njia tofauti. Upanga kama kifaa cha kukata kinalinganishwa na neno la Mungu. Upanga ukiwa na makali hukata chochote bila kuchagua, ilimradi unatumika. Neno la Mungu linalinganishwa na upanga kwa sababu linamhusu mtu yeyote anayelisikiliza ili kumrekebisha dhidi ya maovu bila kuchagua wala kubagua. Kwa hivyo, neno la Mungu ambalo ni maandishi kwenye Biblia Takatifu, linapanuliwa kimaana na kulinganishwa na upanga ambao ni kifaa cha kukatia.

Maana za neno ‘**inua**’ pia zinasawiri upanuzi wa maana. Kuinua ni kuleta juu kitu kilicho mahali palipo chini (TUKI, 2019: 189). Kuinua ni kunyanyua au kuambua kitu, mzigo au hata mkono kutoka katika nafasi ya chini na kusongesha katika nafasi ya juu. Hata hivyo, katika muktadha huu, mhubiri huyu ana maana ya kubadilisha hali duni na kuwa hali bora. Katika hali hii, mhubiri anaamini kuwa Mungu ana uwezo mkubwa wa kumbadilisha mwanadamu kutoka katika hali yoyote, iwe mbaya au duni na kuwa nzuri na bora zaidi.

Neno **‘njia’** linaonekana kupanuliwa kimatumizi. Maana msingi ya neno ‘**njia**’ ni barabara au kichochoro, yaani sehemu inayotumiwa ili kupitia (TUKI, 2019: 490). Barabara humwezesha mtu kutoka mahali fulani kuelekea mahali pengine. Njia pia inaweza kuwa namna au jinsi ya kufanya au kupatia jambo fulani. Hata hivyo, katika muktadha huu, maana ya neno ‘njia’ inapanuliwa vinginevyo. Maana ipatikanayo hapa ni ‘kupitia’ na ‘kuwa mwenye imani kwa Yesu Kristo’. Yaani, katika kumwamini Yesu Kristo unakuwa na matumaini ya

kwenda mbinguni lakini sio kwa njia ya maombi, kutoa fungu la kumi, sadaka na kufunga anavyotaja mhubiri. Wakristo wanaamini kuwa 'kupitia' kwa Yesu Kristo watafika mbinguni na kuishi maisha yasiyo na kikomo.

Vilevile, maneno '**Utu wa kale'** yamehusisha upanuzi wa maana. Katika hali ya kawaida '**utu wa kale'** ni hali inayomwelezea au kumzunguka binadamu aliyeishi zamani, zama zilizopita au siku nyingi zilizopita. Hata hivyo, kwenye muktadha wa mahubiri haya, mhubiri wa 2 ana maana ya 'hali ya uovu' ambayo aghalabu mtu huwa nayo kabla ya 'kuokoka', 'kubadilika' au 'kuzaliwa mara ya pili'. Katika hali hii, 'ukale' au 'uzamani' unalinganishwa na 'uovu' alioufanya mtu kabla hajabadilika na kuwa kiumbe kipya. Muktadha huu wa matumizi ni kubadilika au kuokoka. Maovu kama ukabila, kiburi na kutomsifu Mungu yanatumiwa kwa maana ya 'mambo ya zamani' au 'utu wa kale', wala si 'maovu' ambayo mtu anafanya kabla ya kubadilika. Sio kwamba haya ni maovu ambayo mtu aliyafanya zamani au kale. Kwa hivyo, maana ya 'utu wa kale' inapanuka kimatumizi na kumaanisha 'maovu' au 'utendaji dhambi' kabla ya kubadilika.

Neno '**urembo**' limetumika kwa njia ya pekee ambapo limerudiwarudiwa katika matini ya mahubiri kwa msisitizo. Maana msingi ya nomino '**urembo'** ni uzuri, umaridadi, nakshi au kitu kinachotumika kama pambo (TUKI, 2019: 696). Kwa kawaida, urembo huwa ni wa kuvutia machoni mwa mtazamaji. Hata hivyo, katika muktadha huu, akipanua maana yake, mhubiri wa 3 ana maana ya 'kubadilika kutoka katika hali duni au mbaya na kuwa katika hali bora, maridadi au nzuri'.

Katika mahubiri hayo mapigano ya **vita** yanalinganishwa na hali ya upingamizi au kuzuia kuendelea kwa Injili kwenye muktadha wa mahubiri haya. Maana msingi ya neno **'vita'** ni mapigano baina ya watu, wanyama au mataifa (TUKI, 2019: 716). Kule kuwapiga Wakristo ndiko kulikuwa kunazuia kuenezwa kwa Injili. Maana ya kupigana imepanuliwa kuwa si kupigana halisi bali ni 'kuzuia au kupinga kuenea' kwa Injili katika muktadha wa mahubiri haya.

Dhana hiyo hiyo ya '**pigano**' pia inajitokeza kwa njia nyingine kuonesha 'kupigana na shetani'. Mhubiri huyu ametumia kitenzi '**kupigana**' na shetani ambapo anasema, Mkristo anayetaka kupigana na shetani lazima kwanza ajue maana ya jina lake. Mwanadamu hawezi 'kupigana na shetani' kwa sababu inaaminika kwamba shetani ni roho ambayo haionekani dhahiri na haipatikani katika ulimwengu halisi. Kwa kawaida, kupigana ni kuwa na ugomvi unaosababisha kila mtu kumpiga mwenzake (TUKI, 2019: 527). Hata hivyo, 'kupigana' kunakojitokeza katika muktadha huu ni 'kupingana na kutoshiriki kabisa katika maovu ya kishetani'. Kupigana kwa binadamu na shetani kunafananishwa na mapigano ya kawaida. Dhana ya '**kupigana**' imepanuliwa kimaana na kuwasilisha maana ya 'hali ya kuacha au kujitenga na maovu'.

Kutokana na mahubiri yaliyorekodiwa na kunukuliwa kimaandishi,

imebainika kuwa upanuzi wa maana umejitokeza kwa wingi katika mahubiri yote. Ieleweke kwamba maandiko ya Biblia Takatifu pamoja na mahubiri yanayoambatana nayo, aghalabu, ni matokeo ya tafsiri kutoka lugha moja kwenda nyingine. Matini chanzi ya Biblia Takatifu iliandikwa kwa lugha za Kiebrania na Kigriki (Mojola, 2014). Kwa hivyo, zipo dhana na maneno kwenye mifumo ya lugha za Kiebrania na Kigriki ambazo hazipatikani kwenye mfumo wa lugha ya Kiswahili (Mbiti, 2016). Hali hii aghalabu husababisha upanuzi wa maana za maneno yapatikanayo katika mfumo wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, lugha moja inaweza kuwa na vikoa au msamiati mpana kuliko nyingine kwenye medani fulani ya matumizi. Kwa mfano, katika kuwasilisha ujumbe ambao chanzo chake ni Kiingereza, wahubiri wanaotumia Kiswahili hulazimika kupanua maana ya maneno yaliyomo tayari kwenye mfumo huu. Pamoja na kufanikisha mawasiliano, azma kuu ya lugha kwenye miktadha ya kidini ni kuadilisha na kuwaelimisha waumini kulingana na mazingira yao (Otabek, 2022).

Kimsingi, upanuzi wa maana hufanikisha mawasiliano kupitia maneno kwenye mahubiri hayo. Vilevile, kupanua maana ya usemi ni njia rahisi ya wahubiri kujieleza kwa maneno machache na pia huchochea umakini wa wasikilizaji. Maana ya ziada huathiri dhana, ishara na ujumbe unaobebwa (Jilala, 2017). Sifa za kiisimu na za kiuamilifu hudondoshwa pale ambapo maneno yaliyopanuliwa kimaana huonesha mabadiliko kisematiki. Maana ya maneno yanayohusika huhamishwa na kuwa tofauti kulingana na muktadha wa matumizi bila kubadilika kimatamshi au kimuundo. Hata hivyo, Jilala (keshatajwa) anatahadharisha kwamba huenda uziada ukaathiri upokezi na utambuzi wa ujumbe miongoni mwa hadhira lengwa. Hali hii inatokana na sababu kwamba hadhira ya waumini haipati vionjo wala mtekenyo wa ujumbe ulio sawa. Kuna uwezekano kuwa kwa kiwango fulani kupanuka kwa maana kunaweza kupotosha maana ya maneno mengine na kusababisha ukiushi kimawasiliano.

### 5.2 Ufinyazi wa Maana

Ufinyazi wa maana aghalabu hutokea pale ambapo neno lenye maana pana linatumiwa kuwasilisha maana finyu (Shembilu, 2018). Kwa mujibu wa Wamitila (2008), hali hii hutokea pale ambapo maana ya neno hufinywa na kutumika katika miktadha mingine. Ufinyazi wa kimaana hutokea pale ambapo maana moja maalumu ya neno inatawala na kuishia kuzifanya maana nyinginezo za neno linalohusika kufifia, na labda, hata kupotea kabisa, kama inavyowasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 3:

**Jedwali Na. 3: Ufinyazi wa Maana**

| Msamiati au Neno | Maana ya Kiisimu | Maana ya Kimuktadha |
|---|---|---|
| **Mkubwa** | Kubwa ni yenye kuzidi kwa umbo au kimo; isiyo ndogo. | Kubadilika kutoka kwenye hali duni na kuwa katika hali nzuri ambayo ni bora muhimu na maarufu na muhimu |
| **Ua** | Kufisha au kuondoa uhai. | Kukomesha hali fulani |
| **Roho mtakatifu** | Roho ni nafsi au kitu kisichoonekana, ambacho hufikiriwa kuwa ni sehemu ya mwili wa kiumbe, ambayo hukiwezesha kuwa na uhai; pumzi ya uhai ilhali kivumishi takatifu kina maana ya kutakasika na dhambi au makosa. Kwa hivyo, roho mtakatifu ni nafsi au kitu dhahania kilichotakasika na dhambi ambacho nisehemu ya mwili. | Mungu anayeishi ndani ya Wakristo waliookoka. |

**Chanzo:** TUKI (2019) na Uwandani (2020)

Mathalani, dhana ya **'mkubwa'** inasawiri ufinyazi wa maana. Kivumishi **'kubwa'** kina maana ya 'yenye kuzidi kwa umbo au kimo; isiyo ndogo' (TUKI, 2019: 309). Pia, neno hili lina maana ya 'yenye kwisha kukua au ya juu' (TUKI, 2019: 309). Pamoja na kuonekana kuhawilishwa kutoka kwenye mfumo wa lugha ya Gikuyu (yaani, tafsiri ya maneno, *wi mundu munene*), kauli hii iliyonakiliwa kutoka kwa muktadha wa mahubiri inatumia neno **'mkubwa'** kwa maana ya 'hali kubadilika kutoka kwenye hali duni na kuwa katika hali nzuri ambayo ni bora, muhimu na maarufu.' Kwa hivyo, maana zingine za 'umbo au urefu, upana, miaka mingi' zinatoweka, kisha maana finyu ya 'hali ya juu' kuchukuliwa.

Dhana hiyohiyo ya '**ukubwa**' imetumika kumaanisha 'unene'. Kunenepa ni hali ya kuongezeka na kuwa na umbo pana au kujaa (TUKI, 2019). Viumbe au vitu vingi vinaweza kuwa vikubwa, lakini katika muktadha huu maana ya 'nenepa' imebanika kwenye kanisa ambapo ina maana ya kanisa kuwa na 'idadi kubwa ya waumini' wala sio 'jengo kubwa au kuwepo kwa waumini wanene'.

Kitenzi '**ua**' kimefinyazwa kimaana. Kwa mujibu wa TUKI (2019), '**ua**' ni kitendo cha kufisha au kuondoa uhai wa kitu au mtu. Neno hili limetumika kwa

maana ya ‘kufisha au kukomesha hali fulani.’ Aidha, mhusika anaweza ‘kuua mwenendo au tabia aliyo nayo’. Hali hii ina maana ya ‘kukomesha au kufisha ili isionekane tena’. Katika muktadha huu mhubiri anaacha maana ya ‘kiumbe au binadamu kupoteza uhai’ na kuchukua maana finyu ya ‘kupotea au kukomesha kabisa hivyo kudhihirisha ubanaji wa maana kutokana na maana tambuzi ya kitenzi ‘kuua’ kwa maana ya ‘kuondoa kuwapo kwa uhai wa kiumbe’.

Maneno ‘**roho mtakatifu’** yanasawiri ufinyazi wa maana. Dini zingine kama vile za Kiislamu, Kibahai na Kiyahudi hutumia maneno **‘roho mtakatifu’** kiishara (Badhrulhisham na Hambali, 2018; Krylov, 2019). Katika muktadha huu, roho mtakatifu anaaminiwa kuwa ni Mungu anayeishi ndani ya Wakristo waliookoka na ambaye huathiri mawazo na fikira zao. Pia, Wakristo wanaamini kuwa roho mtakatifu huwapa mwelekeo kuhusu kile wanachopaswa kukifanya. Matumizi ya maneno ‘roho mtakatifu’ yameonesha ufinyazi wa maana kwa mujibu wa mhubiri huyu. Hali hii inaweza kuhusishwa na sababu kwamba dini nyingine pia hutambua roho mtakatifu kwa njia tofauti.

Unapolinganishwa na upanuzi wa maana, mifano iliyochanganuliwa imebainisha kwamba ufinyazi wa maana umejitokeza kwa kiasi kidogo kwenye maneno katika mahubiri ya Kikristo. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyotumiwa na wahubiri ni yenye asili ya lugha za Kibantu, Kiarabu au Kireno. Baadhi ya maneno haya yana vikoa vipana vya maana. Kutokana na hali hiyo, ili mhubiri aweze kuwasilisha ujumbe kamili pasipo kupotosha maana, aghalabu, hulazimika kujibana kwenye maana mojawapo na hivyo kusababisha kufinyazwa kwa maana. Ufinyazi wa maana mara nyingi husababisha taarifa fulani kudondoshwa. Ufinyazi wa maana huenda ukasababisha dhana nzima ya ujumbe ikapotea na hadhira ya waumini ikakosa taarifa muhimu zilizokusudiwa kuwafikia (Jilala, 2017). Hali hii huenda ikasababisha utata katika mawasiliano kwa sababu ufinyazi wa maana katika maneno huenda ukafikishia hadhira ujumbe finyu. Lengo kuu la mhubiri ni kufikia na kuwasiliana na hadhira yake. Kwa hivyo, kama kuna maneno ambayo yanaweza kusababisha utata katika mawasiliano huenda yakaepukwa kimatumizi. Hata hivyo, ni muhali maneno tata kujitokeza katika mahubiri.

### 5.3 Kukisiwa kwa Maana

Ukisiaji wa maana ni hali ya ufasili ambapo neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu kinachohusiana nalo ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Mathalani, dhana ya idadi, kama ilivyojitokeza katika mahubiri yaliyonakiliwa kimaandishi inashadidia ukisiaji wa maana. Tazama Jedwali Na. 4 kwa ufafanuzi zaidi:

**Jedwali Na. 4: Kukisiwa kwa Maana**

| Vifungu vya Maneno | Maana ya Kiisimu | Maana ya Kimuktadha |
|---|---|---|
| **Watu elfu, watu elfu mia tatu, watu milioni moja** | Idadi ya elfu, na milioni | Kuongezeka kwa idadi ya waumini |
| **Billionaire** | Kiasi cha idadi ya mabilioni | Utajiri wa mali nyingi |
| **Msomi wa wasomi** | Mmoja kati ya wasomi | Msomi wa kiwango cha juu zaidi |
| **Barabara ni nyembaba sana na wachache wanaipata** | 'Finyu au yenye kukosa umbo la unene au upana' | Ugumu wa kuingia mbinguni |

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kuna virai kama vile, '***watu elfu elfu, watu elfu mia tatu, watu milioni moja***' ambavyo vimetumiwa kusawiri kuongezeka kwa idadi ya waumini makanisani. Idadi ya juu zaidi inayoonesha kujaa kwa waumini makanisani ni '*watu milioni moja*.' Katika hali halisi ya makanisa haya, huenda hakujawahi kuwa na hakuwezi kuwapo idadi ya watu inayofikia kiwango cha juu kama hicho. Mhubiri huyu ametumia maneno hayo kuonesha kuwa hata watu wajae kanisani na kufika kiwango cha juu zaidi, ni idadi ya wale ambao ni safi tu ndio watakaoingia mbinguni. Kauli hii ina maana kwamba kujaa kwa watu makanisani hakumaanishi kwamba wote wataingia mbinguni. Pia, ni hali ya kusisitiza tu kuwa wahubiri wanapohubiri, wawasisitize waumini kuishi maisha ya kumpendeza Mungu. Azma kuu isiwe kuwavutia waumini ili kujaza kumbi za makanisa yanayohusika. Kwa hiyo, maana halisi ya idadi iliyotajwa sio maana inayotarajiwa kimatumizi katika mahubiri haya.

Kwa kuchanganya Kiswahili na Kiingereza, mhubiri anaishia kukisia maana ya dhana *billionaire*. Kauli hii ina maana kuwa Ayubu, ambaye ni mhusika katika Biblia takatifu, alikuwa na pesa nyingi sana, kwa kiwango cha mabilioni. Maana ya kimuktadha ni kuwa, Ayubu alikuwa na utajiri mwingi sana ambao aliwagawia mabinti zake kwa kiwango cha juu sana. Maana ya dhana ya Kiingereza, *billionaire* sio tu 'kiasi cha pesa' lakini ni 'utajiri wa mali nyingi ya kila aina ambayo haijatajwa'. Mojawapo ya utajiri ambao ametajwa ni *estates*, yaani mashamba, maeneo ya makazi au mali ya mtu binafsi. Kwa hivyo, mali inayorejelewa katika matumizi ya dhana ya Kiingereza *billionaire* kwenye muktadha wa mahubiri haya ni tofauti kimaana.

Kiwango cha usomi wa mhusika kimekisiwa pia katika baadhi ya mahubiri. Hili limetekelezwa kwa uchanganyaji na uhamishaji msimbo. Maneno *'mmoja wa wasomi, na msomi wa wasomi'* yametumiwa na mhubiri kudokeza kiwango cha

masomo cha mhusika ambaye ametajwa. Maneno haya hayabainishi moja kwa moja kiwango chake kamili cha masomo. Hata hivyo, maneno '*msomi wa wasomi*' yametumiwa kuonesha kwamba alikuwa msomi wa kiwango cha juu zaidi kushinda wengine. Huenda ikawa kwamba amefikia upeo wa masomo yote, ama anacho kiwango cha juu zaidi kuliko wasomi wengine.

Wazo la 'uchache' wa waumini wataokaoingia mbinguni siku ya kiama linakisiwa tu kutokana na 'wembamba wa barabara'inayozungumziwa katika mahubiri. Maana ya kivumishi 'nyembamba' ni 'finyu au yenye kukosa umbo la unene au upana' (TUKI, 2019). Barabara ikiwa nyembamba ina maana watakaoitumia ni wachache. Katika dini zilizo nyingi inaaminika kuwa masharti ya kuingia mbinguni sio mepesi. Vilevile, sio watu wengi wanaoweza kutimiza masharti hayo. Inaaminika kuwa huenda wachache tu ndio watakaoweza kufaulu. Maneno 'barabara nyembamba' yametumiwa na mhubiri huyu kuusawiri ugumu wa kuingia mbinguni ambapo ni wachache tu ndio huenda wakafaulu. Hata hivyo, 'wembamba*'* wa barabara hiyo na 'uchache wa watakaoipata' haubainiki katika matumizi ya maneno hayo *'barabara ni nyembamba'* na hivyo kuonesha hali ya kukisia tu.

Yaliyomo kwenye mahubiri ya kidini ni masuala ya imani yanayohusishwa na ukweli. Ukweli huhitaji mantiki, uhakika na usahihi wa kile kinachozungumziwa pasipo ukadiriaji. Hali ya ukadiriaji au ukisiaji huenda ikasababisha utata na upotoshaji wa maana ya ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa. Kimsingi, ukisiaji wa maana husheheni matumizi ya maneno yenye maana tofauti na maana inayojitokeza kwenye muktadha halisi wa mawasiliano. Yamkini, hii ndiyo sababu inayosababisha maneno ya aina hii kutokea kwa uchache kwenye mahubiri mengi. Baadhi ya wahubiri waliochunguzwa hawakuyatumia kabisa.

## 6.0 Hitimisho

Azma kuu ya utafiti huu ni kuchunguza jinsi maana ya maneno yaliyobainishwa kiisimu yanavyorekebishwa kimatumizi kwenye miktadha ya mahubiri ya Kikristo. Makala hii imechanganua kiisimu baadhi ya maneno katika matini ya kidini kwa mtazamo wa Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Utafiti huu umebaini kuwa kuna mabadiliko ya kimaana yaliyojitokeza katika baadhi ya maneno yaliyotumika kwenye mahubiri hayo. Muktadha wa matumizi wa maneno hayo ulionekana kuwa muhimu katika kusababisha athari hizo za mabadiliko ya maana. Utafiti huu ulibaini kuwapo kwa aina kuu tatu za mabadiliko ya kimaana: upanuzi, ufinyazi na ukisiaji wa maana. Hii ni michakato ya kimsingi inayoshughulikiwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika. Maneno mengi yaliyotumiwa na wahubiri yameonesha kupanuka kwa maana na machache ndiyo yameonesha ufinyazi wa maana ilhali kukisiwa kwa maana kumetumika kwa nadra. Matokeo haya yanaakisi tafiti za awali kwenye nyanja kama vile fasihi, jukwaa la mtandao

kijamii wa *Facebook* na elimulahaja inayohusisha lugha za kiasili. Upanuzi na ufinyazi wa maana ndiyo mabadiliko makuu yaliyokithiri katika tafiti nyingi kati ya hizo. Maana msingi na maana za kimktadha zimeonesha mchango mkubwa katika kufanikisha uhusiano wa leksimu kifahiwa. Usawazishaji wa leksimu katika Kiswahili nao umefanikisha uwasilishaji wa maudhui na ujenzi wa wahusika katika baadhi ya riwaya zilizochunguzwa awali. Hata hivyo, tofauti na tafiti za awali, utafiti uliozalisha makala hii umeonesha kwamba matumizi ya maneno yasababishayo mabadiliko ya maana hayafanywi kimakusudi. Mabadiliko hayo yalitokea kisadfa tu ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano kati ya wahubiri na waumini wao. Utoshelevu wa Nadharia ya Pragmatiki Leksika katika kupambanua maana katika mahubiri ya dini ya Kikristo umebainishwa.

**Marejeleo**


Austin, J.L. (1962). *How to Do Things with Words*. Harvard: Harvard University Press.

Badhrulhisham, A. na Hambali, K. (2018). “Konsep Roh Suci Menurut Islam dan Kristian: The Concept of Holy Spirit in Islam and Christian.” *Afkar: Jurnal Akidah & Amp; Pemikiran Islam*. 20(1): 85-108.

Beja, S.K. na Mwinyifaki, A. (2013). “‘Iktibasi’ katika Tenzi za Mwanakupona na Al-Inkishafi”. *Kioo cha Lugha*. 11(1): 30-46.

Blutner, R. (1998). “Lexical Pragmatics”. *Journal of Semantics*. 15: 115-162.

Blutner, R. (2002). “Lexical Semantics and Pragmatics”. *Linguistische Berichte*. 10: 27-58.

Blutner, R. (2004). “Pragmatics and the Lexicon”. Katika L. Hornna G. Ward (Wah.), *The Handbook of Pragmatics*. Oxford: Blackwell. Kur. 488-514.

Blutner, R. (2011). “Some Perspectives on Lexical Pragmatics”. Katika D. Archer. na P. Grundy. (Wah.), *The Pragmatics Reader*. New York: Routledge. Kur. 1-38.

Carston, R. (2002). *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Oxford: Blackwell.

Chembea, S.A. (2020). “Between Charity and Financing ‘Terror’: The Dilemma of Muslim Charitable Organizations in Kenya.” Katika Weiss, H. (h.m), *Muslim Faith-Based Organizations and Social Welfare in Africa*. Cham: Palgrave Macmillan. Kur. 143-168.

Crystal, D. (1966). “Language and Religion.” Katika: Sheppard, L. (Mh.), *Twentieth Century Catholicism*. New York: Hawthorn Books. Kur. 11-28.

Crystal, D. na Davy, D. (2016). *Investigating English Style*. New York: Routledge.

Fairclough, N. (2003). *Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research*. London: Routledge Publishers.

Fairclough, N. na Wodak, R. (1997). "Critical Discourse Analysis'. Katika T. van Dijk. (Mh.), *Discourse as Social Interaction*. London: Sage Publications. Kur. 258-284.

Grice, H.P. (1975). "Logic and Conversation". Katika Cole, P. na Morgan, J. (Wah.), *Syntax and Semantics 3: Speech Acts*. New York: Elsevier. Kur. 41-58.

Grice, H.P. (1989). *Studies in the Way of Words*. Cambridge MA: Harvard University Press.

Halliday, M.A.K. na Hassan, R. (1976). *Cohesion in English*. New York: Longman.

Holmes, J. na Wilson, N. (2022). *An Introduction to Sociolinguistics, Toleo la 6.* New York: Routledge.

Indede, N.F. (2007). *Lugha ya Kitamathali katika Mahubiri ya Dini ya Kikristo*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno.

Jilala, H. (2017). "Matatizo ya Tafsiri katika Matini za Kitalii nchini Tanzania". *Kioo cha Lugha.* 12(1):1-22.

Katz, J.J. na Fodor, J.A. (1963). "The Structure of a Semantic Theory". *Language*. 39:170-210.

Kevogo, A.U. (2020) *Nafasi ya Mielekeo katika Uteuzi wa Lugha: Mfano wa Matumizi ya Lugha katika Mahubiri ya Kikristo Jijini Nairobi*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Kevogo, A.U. na Kevogo, S.A. (2018). "Matumizi ya Lugha katika Mitandao ya Kijamii: Mfano wa Kiswahili katika Blogu za Kikristo". Katika M. Mukuthuria. na M. Kandagor . (Wah.), *Lugha ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo yake*. Dar es Salaam: TUKI na Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki. Kur. 215-233.

King'ati, J. (2002). *Discourse Analysis in Swahili Homilies*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI.

Krylov, G. (2019). "The Holy Spirit as seen through the prism of Islam." *Issues of Theology*. 1(4): 576-590.

Malugu, A. (2016). "Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri Suala la Dini". *Kiswahili. 79*(1): 66-77.

Marisya, P. (2017). *Mchango wa Sajili ya Kidini katika Kufanikisha Riwaya Mbili za Ken Walibora* (*Kidagaa Kimemwozea* na *Ndoto ya Almasi*). Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J. (2016). "Main Features of Twenty-First Century Christianity in Africa". *Missio Africanus Journal of African Missiology*. 1(2): 72-88.

McCawley, J.D. (1978). "Conversational Implicature and the Lexicon". Katika P. Cole. (Mh.), *Syntax and Semantics 9: Pragmatics*. New York: Academic Press. Kur. 245-259.

Mojola, A.O. (2014). The Old Testament or Hebrew Bible in Africa: Challenges and Prospects for Interpretation and Translation. *Verbum et Ecclesia.* 35(3):1-7. https://hdl.handle.net/10520/EJC160049.

Mpalanzi, L.E. (2019). "Makutano kati ya Dini ya Jadi na Dini za Kigeni: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili". *Kioo cha Lugha.* 17(1):114-131.

Mutiso, K. (1996). *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kaswida ya Burudai*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziya*. Dar es Salaam: TUKI.

Nthenya, E. (2012). *Communication Strategies by Interpretors from Selected Pentecostal Churches in Machakos Town, Kenya*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Odhiambo, K., Musyoka, E.N. na Matu, P.M. (2013). "The Impact of Consecutive Interpreting on Church Sermons: A Study of English to Kamba Interpretation in Machakos town, Kenya". *International Journal of Academic Research in Business & Social Sciences*. 3(8):189-204. http://dx.doi.org/10.6007/IJARBSS/v3-i8/136.

Ogonda, J.E. (1998). *Matatizo ya Ukalimani: Uchambuzi wa Mahubiri ya Kidini*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogutu, O.G. (2013). *Athari za Sheng katika Dini ya Kikristo: Mtaa wa Umoja*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Okombo, L. (2011). *Sitiari, Taashira na Tashbiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utenzi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimtindo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Osore, M. (2015). "Fasihi Andishi ya Kiswahili na Dini: Mifano ya Riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi". Makala iliyowasilishwa katika Kongamano la Kimataifa la Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA), Chuo Kikuu cha Mount Kenya. http:// erepository.mku .ac.ke/handle/123456789/87

Otabek, B. (2022). "Stylistic Features of Representation of Religious Vocabulary in Modern Linguistics". *Galaxy International Interdisciplinary Research Journal.* 10(11):1145-1149. https:// giirj.com/index.php /giirj/article/view/3946.

Searle, J. (1969). *Speech Acts: An Essay in the Philosophy of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Shembilu, M.M. (2018). "Misigano baina ya Maana ya Asili na Maana ya Sasa kwa Baadhi ya Nomino zenye Asili ya Kiarabu katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2004)". *Kioo cha Lugha.* 7(1):11-16.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Waweru, T. (2014). *Matumizi ya Lugha katika Kanisa Katoliki: Uchanganuzi wa Ubadilishaji Msimbo katika Mahubiri*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wilson, D. (2003). "Relevance and Lexical Pragmatics". *Italian Journal of Linguistics.* 15: 273-292.